JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAFUNZO YA VIONGOZI KATIKA NGAZI YA KIJIJI, MTAA NA KITONGOJI

MKAKATI WA KUPAMBANA NA RUSHWA KATIKA NGAZI YA KATA, KIJIJI KITONGOJI NA MTAA

9

DODOMA
APRILI, 2001

YALIYOMO

Uk.

1. Utangulizi 1

2. Kwanza tujiulize Rushwa ni Nini.....1

3. Matumizi mabaya ya Ofisi za Umma..... 2

4. Majukumu ya Viongozi katika Serikali za Kata, Kijiji, Kitongoji za Mtaa.....3

MKAKATI WA KUPAMBANA NA RUSHWA KATIKA NGAZI YA KATA, KIJIJI, KITONGOJI NA MTAA

1. UTANGUIZI

Watumishi wa ngazi zote za Serikali za Mitaa wanapaswa kuwa waadilifu, waaminifu na wenye kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Halmashauri zao na kwa wananchi walipa kodi ambao wanawajibika kwao. Kimsingi mishahara ya viongozi wa ngazi zote inatokana na kodi za wananchi.

Ili kuboresha huduma kwa wananchi ambao ndiyo walipa kodi ni jukumu la viongozi kuanzia ngazi ya chini hadi Taifa kuwa waadilifu, waaminifu na wanyenyekevu wakati wa kutoa huduma ili wananchi waondokane na umaskini.

Moja ya mambo ambayo yanasababisha kero kwa wananchi vijijini na mitaani mpaka ngazi ya juu ni pale ambapo mtumishi na viongozi wa Serikali za Vijiji, Vitongoji, Mitaa na Kata wanajiingiza katika vitendo vya rushwa na kushindwa kujenga mazingira mazuri yenye kumuwezesha mwananchi kujikwamua kutokana na umaskini.

2. Kwanza tujiulize Rushwa ni nini?

Si rahisi kutoa tafsiri ya moja kwa moja au maana halisi ya dhana ya rushwa kwa vile kuna aina mbalimbali ya vitendo vinavyohesabika kuwa ni rushwa. Ugumu huu umechangiwa na tofauti iliyopo kati ya jamii moja na nyingine kuhusu maana ya rushwa, na ndio maana dhana ya rushwa imepachikwa majina mbalimbali kulingana na mabadiliko ya nyakati au tofauti ya mazingira miongoni mwa jamii. Wapo watu ambao wanaiita mchicha, mlungula, fadhila, soda na chauchau. Wengine rushwa inaitwa chai, kitu kidogo, kifuta jasho na mengine mengi. Lakini majina yote haya yana-

maanisha kitu chochote cha kuweza kumshawishi mtumishi wa umma aweze kufanya au asifanye kitu ambacho alitakiwa kufanya au asifanye kwa mujibu wa sheria za nchi zilizopo na hivyo kujipatia kipato cha ziada ya kile ambacho anastahili kupata kwa nafasi yake na kwa mujibu wa sheria inayomuongoza katika utendaji wake. Pamoja na tafsiri za rushwa kuwa nyingi kwa kifupi maana nyepesi na rahisi kuelezea rushwa ni matendo ya kiongozi na mtumishi wa umma ya kutumia nafasi aliyonayo (cheo au wadhifa) kwa manufaa yake binafsi. Rushwa ni pamoja na kupindisha Kanuni, Taratibu, Sheria za nchi kwa nia ya kujipatia manufaa binafsi. Hii inajumuisha pia wale wote wanaopenda kutumia fedha au chochote ili mtoa huduma afanye wanavyotaka wao.

Rushwa inaweza pia kutafsiriwa kama uvunjaji au mmomonyoko wa maadili katika misingi ya upendeleo au undugu, mathalani katika kutatua migogoro ya ardhi, maswala ya ndoa, na makosa mengine madogo madogo ambapo viongozi wa Vijiji na Kata wanatakiwa kuwa waadilifu na wenye kuzingatia maadili husika na kutotumbukia katika mtego wa kusaidia kwa sababu ya undugu au upokeaji wa fedha kama rushwa. Rushwa pia ni tabia ya kutowajibika, kutofuata Sheria, Taratibu au Kanuni za kazi kwa misingi ya kutaka kujinufaisha.

3. Matumizi mabaya ya Ofisi za Umma.

Katika ngazi ya Kijiji, Mtaa na Kitongoji viongozi waliopewa jukumu la kuendesha Serikali ya Kijiji ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Mtaa na Kitongoji sawia. Katika maeneo ya vijijini Afisa Mtendaji wa Kijiji ni Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji. Ipo Kamati ya maendeleo ya Kata ambayo inaratibu shughuli za maendeleo katika Kata. Mwenyekiti wa Kamati

hii ni Diwani na Katibu wa Kamati ya Maendeleo ya Kata ni Afisa Mtendaji wa Kata. Uongozi wa Vijiji na Kata, pamoja na mambo mengine, unasimamia leseni za biashara, ugawaji wa mashamba, ukusanyaji wa kodi na ushuru mbalimbali. Aidha, wakati wa utendaji wao wa kazi hutokea mgongano baina ya wanavijiji wenyewe au hata na Serikali yao ya Kijiji, Mtaa hadi Kata.

Mtumishi mmojawapo au kwa kushirikiana na viongozi wa kisiasa wakitumbukia katika vitendo vya rushwa hutumia Ofisi ya umma kwa manufaa binafsi na hivyo hushindwa kwa mfano kukusanya mapato ya leseni za biashara, ushuru na hushindwa kushughulikia ugawaji wa mashamba kwa haki na hata kutatua migogoro kwa upendeleo.

4. Majukumu ya Viongozi Katika Ngazi ya Kata, Kijiji, Kitongoji na Mtaa

Viongozi wa Vijiji, Vitongoji, Mitaa na Kata wanatakiwa wawajibike kwa Halmashauri zao na wananchi kwa ujumla kwa kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni za kazi zao. Kuwajibika ni pamoja na kuitisha vikao ambavyo vinatakiwa kulingana na Kanuni za Halmashauri.

Kusimamia kwa ukamilifu ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ushuru, leseni na kutatua migogoro kulingana na sheria, kanuni, mila na desturi nzuri kama zinavyotambuliwa na jamii.

Viongozi ngazi ya Vijiji, Vitongoji, Mtaa na Kata wanatakiwa wawe mstari wa mbele katika vita dhidi ya rushwa kwa kufanya mambo yafuatayo:-

a) Kusimamia na kuchochea juhudi za wananchi kujiletea na kujiongezea maendeleo ya mtu mmoja mmoja, Kijiji, Kata na kuendelea. Hili linawezekana

pale ambapo hakuna rushwa, migogoro ya ardhi, wizi wa fedha zinazokusanywa kama ushuru na michango ya Wanavijiji.

b) Kusimamia kwa usawa na haki huduma zinazohusu maisha ya watu ya kila siku kama vile Usalama, Afya ya msingi, Elimu, Ujenzi na matengenezo ya barabara za Vijijini. Haya yanawezekana kama Sheria, Kanuni na Taratibu za huduma hizo zikifuatwa bila upendeleo, undugu au ubinafsi.